Jarida la

# SIHA NA MAENDELEO

UTAWALA BORA

www.sihadc.go.tz | Mwezi Novemba 2023 | Toleo la 11 | Halmashauri ya Siha



## CHANGAMOTO YA KUKOSEKANA MAJI SIHA SASA KUPATIWA SULUHU – RC KILIMANJARO



**Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe. Nurdin Babu akizungumza kwenye mkutano wa dharura wa baraza la Wah. Madiwani lililofanyika Novemba 14, 2023 katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha kilichokuwa na lengo la kujadili changamoto ya uhaba wa maji inayosababishwa na ongezeko kubwa la watu Wilaya ya Siha, Mkoa wa Kilimanjaro**

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe. Nurdin Babu amemuelekeza Meneja wa Wakala na Maji na Usafi wa Mazingira (RUWASA) Mkoa kufika wilaya ya siha kubaini na kushughulikia changamoto ya baadhi ya wananchi kukosa maji hasa nyakati za ukame.

Mhe Babu ametoa maelekezo hayo Novemba 14, 2023 kwenye Mkutano wa Dharura ya wa Baraza la madiwani uliofanyika kwenye Ukumbi Mkubwa wa Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha kwa lengo la kujadili changamoto ya uhaba wa maji inayosababishwa na ongezeko la Wakazi Wilaya ya Siha.

Amesema wananchi na wakazi wa wilaya ya siha hawahitaji maneno bali wanahitaji maji hivyo suala la maji halina mjadala kwani adhma ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan na Waziri wa Maji ni wananchi wapate huduma ya maji Safi na Salama.

“Kwa hiyo Meneja wa RUWASA Mkoa, nataka mfike hapa mshirikiane na wenzenu wa wilaya kubaini changamoto na kuzishughulikia wananchi wapate maji, mimi nitakuja hapa kukagua kazi zilizofanyika” amesema Mhe. Nurdin Babu, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro.





*Naibu Waziri wa Afya na Mbunge wa Jimbo la Siha Mhe. Dkt Godwin Mollel (picha ya kushoto) na Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe. Dkt Christopher Timbuka (picha ya kulia) wakizungumza katika kwenye mkutano wa dharura wa baraza la madiwani uliofanyika Novemba 14, 2023 katika ukumbi mkubwa wa makao makuu ya halmashauri ya wilaya ya siha kilichokuwa na lengo la kujadili changamoto ya uhaba wa maji inayosababishwa na ongezeko la wakazi wa wilaya ya siha, Mkoa wa Kilimanjaro*










*Baadhi ya viongozi wa Mkoa na Wilaya na Wataalamu walioshiriki kwenye mkutano wa Dharura wa Baraza la Madiwani uliofanyika Novemba 14, 2023 katika ukumbi mkubwa wa makao makuu ya halmashauri ya wilaya ya siha.*

## MKUU WA WILAYA YA SIHA MHE. DKT. TIMBUKA AWAELEKEZA VIONGOZI WA VYAMA VYA USHIRIKA KUFUATA SHERIA, KANUNI, TARATIBU



*Mkuu wa Wilaya ya Siha* **Mhe. Dkt Christopher Timbuka** *akizungumza kwenye kikao kazi na viongozi wa vyama vya ushirika Wilaya ya Siha kilichofanyika kwenye Ukumbi Mkubwa wa Makao Makuu ya Halmashauri ya Siha Novemba 16, 2023*

Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe. Dkt Christopher Timbuka amewaelekeza viongozi wa vyama vya ushirika Wilaya ya Siha kufanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zinazowaongoza ikiwemo kuwasomea taarifa za mapato na matumizi wanachama.

Mhe. Dkt Timbuka ametoa maelekezo hayo Novemba 16, 2023 kwenye kikao kazi na viongozi wa vyama vya ushirika Wilaya ya Siha kilichofanyika kwenye Ukumbi wa Makao Makuu ya Halmashauri ya Siha ambapo lengo la kikao ni kujadili changamoto, mafanikio na mikakati ya kuboresha vyama vya ushirika.

Amesema viongozi wa vyama vya ushirika wakifanya kazi zao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu ikiwa ni pamoja na kufanya vikao vilivyopo kikanuni, kusoma mapato na matumizi ya vyama kwa uwazi na kuwashirikisha katika maamuzi yanayohusu mali za chama kutasaidia kwa kiasi kikubwa kumaliza migogoro ndani ya vyama vya ushirika.

Amesema wafanyabiashara wa Wilaya ya Siha na nje ya Wilaya wanatakiwa kuongeza kasi ya kuja kuwekeza ndani Wilaya ya Siha kwani fursa zipo nyingi ili kukuza uchumi.

“Maeneo ya uwekezaji katika Wilaya ya Siha yapo mengi ikiwa ni pamoja na maeneo ya watu binafsi,maeneo ya ushirika pamoja na maeneo maalum yaliyotengwa na Halmashauri ya Siha” Amesema Dkt Timbuka






*Baadhi ya Viongozi wa vyama vya Ushirika wakitoa ushauri na mapendezo ya kuboresha vyama vya ushirika Wilayani Siha ukumbi wa Halmashauri Novemba 16, 2023*




*Baadhi ya viongozi wa vyama vya ushirika Wilayani Siha walioshiriki katika kikao kazi na Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe. Dkt Christopher Timbuka kwa lengo la kujadili Changamoto, Mafanikio na Mikakati ya kuboresha vyama vya ushirika*

## WAKULIMA SIHA WATAKIWA KUTUMIA MBINU BORA ZA KISASA ILI KUONGEZA UZALISHAJI WA MAZAO



**Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Haji M. Mnasi,PhD akizungumza kwenye mahafali ya pili na maonesho ya vikundi vya wakulima wa RIPAT Wilaya ya Siha yaliyofanyika katika Kiwanja cha Fuka, Kata ya Kirua.**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Haji M. Mnasi,PhD amevitaka vikundi vya wakulima wa RIPAT vilivyopo katika Kata Sita za Wilaya ya Siha kutumia na kueneza mafunzo ya kuboresha kilimo kwa kuzalisha mazao mengi na bora kwa kuzingatia teknolojia za kisasa kwenye eneo dogo la ardhi ili njaa na umaskini iwe historia.

Mnasi (PhD) ametoa rai hiyo Novemba 11, 2022 katika mahafali ya pili na maonesho ya vikundi vya wakulima wa RIPAT Wilaya ya Siha yaliyofanyika katika kiwanja cha Fuka huku akiongeza kuwa mafunzo hayo yanayotolewa na Shirika la KIWAKKUKI yawe yenye tija katika uzalishaji wa mazao mengi na bora ili kuimarisha upatikanaji wa chakula.

Ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa mvua hali inayosababisha wakulima kuvuna mazao kidogo, Mkurugenzi Mtendaji Haji M. Mnasi (PhD) amesema Serikali kupitia tume ya taifa ya umwagiliaji katika mwaka fedha 2023/24 imepanga kuchimba visima 150 kwa ajili ya Kilimo cha umwagiliaji ndani ya Wilaya.

Pia amesema Halmashauri inaendelea na uchimbaji wa mifereji ya umwagiliaji Mitimirefu na Ngaroni ili kurahisha upatikanaji wa maji kwa ajili ya umwagiliaji na Serikali itaendelea na uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji.

Jumla ya Vikundi 41 vyenye wakulima 986 wakiwemo wanafunzi 199 wa Shule za Sekondari wamewezeshwa kutumia teknolojia mbalimbali za kilimo cha kisasa na ufugaji bora tangu Mwaka 2020 kwa nadharia na vitendo katika maeneo ya shamba darasa.



*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Haji M. Mnasi (PhD) akitazama mazao ya Vikundi vya wakulima wa RIPAT katika Mahafali ya Pili na Maonesho ya Vikundi vya Wakulima wa RIPAT Wilaya ya Siha yaliyofanyika katika kiwanja cha Fuka katika Kata ya Kirua.*



*Mkurugenzi Mtendaji  Halmashauri ya Wilaya ya Siha Haji M. Mnasi (PhD)  akitazama Mashamba ya Darasa ya Vikundi vya wakulima wa RIPAT katika Mahafali ya Pili na Maonesho ya Vikundi vya Wakulima wa RIPAT Wilaya ya Siha yaliyofanyika katika kiwanja cha Fuka katika Kata ya Kirua.*

# HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA YASHIKA NAFASI YA PILI UKUSANYA YA MAPATO MKOA WA KILIMANJARO




*Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya* ***Siha*** **Mhe. Duncan Urassa** *(katikati) akizungumza kwenye Mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani kipindi cha Robo ya kwanza ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 uliofanyika Novemba 7, 2023 katika Ukumbi Mkubwa wa Mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha.*

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Mhe Duncan Urassa amempongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Haji M. Mnasi (PhD) na timu yake ya wataalamu kwa kuiwezesha Halmashauri kuwa katika nafasi ya pili Kimkoa kwenye ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha.


Mwenyekiti Mhe.Urassa ametoa pongezi hizo novemba 07, 2023 kwenye Mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani wa Robo ya kwanza ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 uliofanyika katika Ukumbi Mkubwa wa Mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha.

Mhe. Urassa amewaomba waheshimiwa Madiwani kuendelea kutoa ushirikiano kwa wataalamu ili kufikia makisio ya makusanyo ya mapato ya ndani ya mwaka huu wa fedha.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Haji M. Mnasi (PhD) amewahakikishia Waheshimiwa Madiwani na Wananchi wa Wilaya ya Siha kuwa Halmashauri itaendelea kusimamia kwa ufanisi na weredi ukusanyaji wa mapato ili kufanya vizuri zaidi hali itakayochochea uboreshaji wa huduma zinazotolewa kwa Wananchi.





*Waheshimiwa madiwani, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha na Wataalamu wakiwa kwenye Mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani wa Robo ya kwanza ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 uliofanyika Novemba 7, 2023 katika Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha.*

# WILAYA YA SIHA YAPOKEA SHILINGI BILIONI 2.79 ZA MIRADI YA MAENDELEO NOVEMBA 2023



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Haji M. Mnasi, PhD anawajulisha Wananchi, Wakazi wa Wilaya ya Siha na Watanzania kwa ujumla kuwa mwezi Novemba 2023 Halmashauri ya Wilaya ya Siha imepokea fedha za miradi ya maendeleo jumla ya Shilingi 2,792,650247.00 **(Bilioni mbili, Milioni Mia Saba Tisini na Mbili, Laki Sita na Elfu Hamsini Mia Mbili Arobaini na Saba Tu)** kutoka Serikali ya awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Aidha fedha hizi za miradi ya maendeleo zitatumika katika kujenga miundombinu mipya katika sekta ya Afya, Elimu Msingi, Elimu Sekondari pamoja na kununua Vifaa Tiba vya kuboresha utoaji wa huduma za Afya kwa Jamii.

Mchanganuo wa Miradi ya Maendeleo itakayotekelezwa pamoja na kiasi kitakachotumika Imeambatishwa kwenye jedwali hapo chini:

| Na | Miradi | Idadi ya Miundombinu | Jumla ya Fedha |
|---|---|---|---|
| 1 | Shule Kongwe za Msingi | Ujenzi Wa Vyumba 9 Vya Madarasa katika Shule Kongwe za Msingi | 180, 000, 000 |
| 2 | Matundu ya Vyoo Shule za Msingi | Ujenzi wa Matundu 10 ya Vyoo katika Shule ya Msingi Sanya Juu | 28,000,000 |
| 3 | Bweni | Ujenzi wa Bweni la wanafunzi wenye Mahitaji Maalum Shule ya Msingi Ormelili | 128,000,000 |
| 4 | Vifaa Tiba | Ununuzi wa Vifaa Tiba Hospitali ya Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati | 900,000,000 |
| 5 | Zahanati | Ukamilisha ujenzi wa Zahanati ya Mawasiliano na Mowonjamu | 100,000,000 |
| 6 | Vyumba vya Madarasa Kidato cha Tano | Ujenzi wa Vyumba vya Madarasa 48 katika shule 10 za Sekondari Kidato cha Tano | 1,196,000,000 |
| 8 | Matundu ya Vyoo Kidato cha Tano | Matundu 125 ya Vyoo katika shule 13 za Sekondari kidato cha Tano | 138,000,000 |
| 9 | Mfuko wa Jimbo | Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Mfuko wa Jimbo | 58,297,000 |
| 10 | Mfuko wa Pamoja wa Afya (Health Social Basket Fund – HSBF) | Kuwezesha utekelezaji wa huduma za afya katika vituo vya kutolea huduma. | 64,353,247 |
| **TOTAL** | | | **2,792,650247.00** |

Aidha, Dkt. Mnasi ameishukuru Serikali ya awamu ya sita kwa kuleta fedha nyingi za miradi ya maendeleo na ametoa wito kwa watumishi wa Umma kusimamia fedha hizo vizuri ili kutimiza malengo yaliyokusudiwa.

SIHA NA MAENDELEO

**TUSAIDIENI KUKUSANYA NA KUJADILI TAARIFA ZA MAPATO KWENYE KATA ZENU – HAJI MNASI, PhD**



*Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Siha Haji Mnasi PhD akizungumza kwenye Mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani kipindi cha Robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2023/24 uliofanyika Novemba 07, 2023 katika wa Halmashauri ya Siha.*

SIHA DC

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Haji Mnasi (PhD) amewaomba waheshimiwa madiwani kuendelea kushirikiana na watendaji wa kata ili kukusanya na kujadili taarifa za mapato kwenye ngazi za chini na kuzitafutia ufumbuzi changamoto zinazojitokeza ndani ya kata.

Mnasi (PhD) ametoa ombi hilo Novemba 07, 2023 wakati akizungumza kwenye Mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani wa Robo ya kwanza ya Mwaka wa Fedha 2023/24 uliofanyika Novemba 07, 2023 katika Ukumbi Mkubwa wa Makao Makuu ya Halmashauri ambapo amesema Waheshimiwa Madiwani wakiendeleza ushirikiano hakuna chanzo hata kimoja cha mapato katika kila eneo ndani ya Halmashauri kitarukwa.

Amesema Menejimenti ya Halmashauri itaendelea kutoa ushirikiano wa karibu ili kuiwezasha Halmashauri kushika nafasi ya kwanza Kimkoa kwenye ukusanyaji wa mapato ya ndani katika robo ya pili ya mwaka huu wa Fedha.




*Baadhi ya Viongozi wa Serikali Mkoa na Wilaya, Chama Tawala na Taasisi za Serikali wakichangia mjadala kwenye Mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani Robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2023/24 uliofanyika Novemba 07, 2023.*



*Waheshimiwa Madiwani wakiwa kwenye Mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani wa Robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2023/24 uliofanyika Novemba 07, 2023 katika Ukumbi Mkubwa wa Makao Makuu ya Halmashauri ya Siha.*

Mkurungenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha 5-BR Elerai- Sanya Juu S.L.P 129,25482 siha Simu Na +027-2970677, Nukushi +027-2970677 Barua Pepe: ded@sihadc.go.tz, Tovuti: www.sihadc.go.tz

# WATUMISHI SIHA WAANZA KUTUMIA MFUMO WA PEPMIS




*Mkurugenzi wa Mipango Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Cosmas Ngangaji akizungumza wakati wa kufungua mafunzo ya kutumia mfumo mpya wa usimamizi wa utendaji kazi kwa watumishi wa umma (PEPMIS) yaliyofanyika Novemba 23, 2023 Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha.*

Mkurugenzi wa Mipango Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Cosmas Ngangaji amewataka watumishi wa Wilaya ya Siha kuanza kutumia mfumo mpya wa usimamizi wa utendaji kazi kwa mtumishi wa umma (PEPMIS) ili kuboresha utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa umma.

Mkurugenzi Ngangaji ametoa wito huo Novemba 23, 2023 baada ya mafunzo ya kuutumia mfumo huo mpya wa PEPMIS unaochukua nafasi ya mfumo wa wazi wa upimaji wa utendaji kazi kwa watumiashi wa umma (OPRAS)uliokuwa ukitumika awali yaliyofanyika katika ukumbi wa Mikutano wa Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha.

Amesema mfumo huo mpya utasaidia kufanya tathmini ya rasilimali watu katika halmashauri ili kujua ziada na upungufu uliopo katika maeneo mbalimbali kwa kuangalia muda na utalaamu walionao watumishi wa umma.

“Kama serikali tunakuja na mfumo ambao utatusaidia kufanya maamuzi ya ajira mpya zinazohitajika na uhamisho ili kuhakikisha kwamba rasilimali watu zinakaa panapotakiwa na kwa idadi inayotakiwa” amesema Mkurugenzi wa Mipango Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Cosmas Ngangaji

# HABARI PICHA ZA MIRADI YA MAENDELEO WILAYA YA SIHA







*Muonekano wa Shule mpya ya Awali na Msingi Munge iliyotekelezwa kwa Fedha Shilingi Milioni 250 kutoka Serikali Kuu, Shilingi Milioni 12.22 za Mapato ya ndani ya Halmashauri na Shilingi Milioni 20.73 za Michango na nguvu za Wananchi katika Kijiji cha Munge, Kata ya Donyomurwak Wilaya ya Siha.*

## SHULE YA SEKONDARI SANYA JUU KATA YA NASAI







*Mwonekano wa mabweni mawili mapya, Vyumba saba vya madarasa na matundu 14 ya vyoo katika shule ya* **Sekondari Sanya Juu** *iliyopo katika Kata ya Nasai Wilaya ya Siha yaliyotekelezwa kwa fedha* ***shilingi milioni 464.4*** *kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya kidato cha tano mwaka 2023.*

## HOSPITALI YA WILAYA YA SIHA ILIYOPO KATA YA SANYA JUU



*Mwonekano wa Hospitali ya Wilaya ya Siha baada ya kujengwa njia za kutembelea (Walk Ways) kuunganisha Majengo ya Hospitali, Jengo la Upasuaji, Wodi ya Wananume na Wodi ya Magonjwa Maalumu ya Wanawakeambayo yametekelezwa kwa fedha shilingi Milioni 800 kutoka serikali kuu.*

## MADARASA MAPYA NA MATUNDU YA VYOO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KARANSI



*Muonekano wa madarasa mapya na Matundu ya Vyoo katika shule ya sekondari Karansi yaliyotekelezwa kwa fedha shilingi milioni 466.5 kutoka serikali kuu kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya kidato cha tano kwa mwaka 2023 zilizoelekezwa kujengwa Mabweni Mawili, Vyumba Saba vya Madarasa na Matundu 15 ya Vyoo.*



*Muonekano wa Vyumba Vinne vya Madarasa vya mradi wa BOOST katika Shule ya Awali na Msingi Ngaremji ambapo shule ilipokea shilingi Milioni 106 kwa ajili ya ujenzi wa Vyumba Vinne vya Madarasa na Matundu Matatu ya Vyoo.*

## FURSA ZA UTALII KATIKA WILAYA YA SIHA MKOA WA KILIMANJARO










*Tembelea Maporomoko ya West Kilimanjaro, Fahari ya Wilaya ya Siha Mkoa wa Kilimanjaro na Tanzania kwa ujumla*

















**JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**

**Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha**
**5-BR Elerai- Sanya Juu S.L.P 129,25482 siha**
**Simu Na +027-2970677, Nukushi +027-2970677**
**Barua Pepe: ded@sihadc.go.tz, Tovuti: www.sihadc.go.tz**

**Tunapatikana**